



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA



**HALMASHAURI YA WILAYA YA MLELE**

## **TANGAZO LA FURSA ZA MIKOPO**

18 Oktoba 2021

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mlele anapenda kuwatangazia vikundi vya Wanawake, Vijana na Watu wenye Ulemavu vilivyo na sifa za kupata mikopo isiyo na riba kwa mwaka wa fedha 2021/2022, kuwa Halmashauri imeanza kupokea maombi ya mikopo hiyo kwa robo ya pili (Oktoba - Desemba 2021), ambayo ni asilimia 10 ya mapato ya ndani. Hivyo vikundi vinatakiwa kuwasilisha maombi ya mikopo, maombi hayo yathibitishwe katika ngazi ya kijiji na kata kabla ya kufikishwa ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji. Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 31 Desemba 2021 saa 9:30 alasiri.

### **VIGezo**

1. Kikundi kiwe kimesajiliwa kutoka ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji
2. Kikundi kiwe na katiba inayoonesha uendeshaji wa shughuli zake
3. Kikundi kiwe na mradi unaomilikiwa na kusimamiwa na wanakikundi wote na sehemu maalum inayotambulika ya shughuli zao
4. Umri wa vikundi vya vijana ni kuanzia miaka 18 - 35
5. Kikundi lazima kiwe na akaunti namba ya benki
6. Idadi ya wanachama wa vikundi vya wanawake na vijana ni kuanzia watano (5) na kuendelea, watu wenye ulemavu ni kuanzia mtu mmoja.

### **VIAMBATANISHO**

1. Nakala ya cheti cha usajili wa kikundi
2. Nakala ya fomu ya Malipo ya Benki (Bank Slip) inayoonesha akaunti namba ya kikundi
3. Mhutasari wa kikao cha kikundi wenye maombi ya mkopo na mfumo wa urejeshaji
4. Fomu ya maombi ya mkopo (inapatikana ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji na ofisi ya Kata au kwenye tovuti ya halmashauri ([www.mleledc.go.tz](http://www.mleledc.go.tz)))
6. Mchanganuo wa mradi ulioombewa na kiasi cha mkopo (kwa ufafanuzi zaidi fika ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji - Idara ya Maendeleo ya Jamii).

**MUHIMU: MIRADI INAYOLENGA UANZISHWAJI AU UENDELEZAJI WA VIWANDA VIDOGO VITAKAVYOONGEZA AJIRA NA TIJA ITAPEWA KIPAUMBELE**

  
Teresia A. Irafay  
Mkurugenzi Mtendaji (W)  
Halmashauri ya Wilaya ya Mlele

**MKURUGENZI MTENDAJI  
HALMASHAURI YA (W) MLELE**